# MAELEZO YA IBADA YA KILUTHERI

# AGIZO LA MEZA YA BWANA

KWA SABABU KILA MARA MNAPOKULA MKATE HUU, NA KUNYWA KIKOMBE HIKI, MNATANGAZA KUFA KWA BWANA HATA HATAKAKUJA

1 Corintho 11 : 26

# MAELEWO YA IBADA YA KILUTHERI AGIZO JUU YA MEZA YA BWANA

Tendo « *Liturgia* » maana yahe « kazi ao kutumikia » katika maisha yetu mazima kama wakristo wanapashwa kuwa watu wenye kumtumikia Mungu. Ni mu kazi ya siku ya juma, kwa hiyo, kutumikia ao kazi ya juma, kwa hiyo, kutumikia ao kazi ya maisha yetu ya Kikristo inakuwa mu furaha mkubwa, inakuwa kwetu inasema nasi, na inatubariki kupitia neno na sakramenti yake. Tunaenda kwake naye tunasema kupitia sala zetu na sifa. Kazi ya kuabudu siku ya juma ni wakati mzuri sana ndani ya maisha yetu hapa duniani.

## I. TUNAJITAYARISHA KWA KUKUTANA NA MUNGU

Mkristo anaombwa kufika mbele ku ibada ya kwabudu. Hii ni wakati wa kujitayarisha.

Wakati wa kwenda mbali, kuondosha mawazo mbali mbali ya kidunia ao maisha, na ya kazi : ujitayarishe uwe pekee yako juu ya ibada ya Mungu wako hata hivi kwa kusikia na kufunda neno lake tukisoma zaburi moja. Tazama na usome maandiko ao barua ya mafundisho, nyimbo za siku.

**Wimbo wa kiingilio**

Tunaangaza kazi ya ibada tukimuimbia Bwana mimbo wa sala.

**Ombi la utatu mutakatifu** (P 15)

Na hii tunatoa akikisho kama tuna 'abudu utatu mtakatifu na Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Tunaomba utatu mtakatifu kwa kuwa nasi na kutubariki kama vile tunafanya ibada yetu.

**KUTUBU ZAMBI NA MAONDELEO AO MSHAMAHA WA ZAMBI** (P. 15)

Mbele tunapaswa kujishusha juu ya kumwabudu Mungu wetu mtakatifu, kwanza kabisa tunapashwa kutosha ma zambi yetu. Kwa hiyo tuna kuja kwake kwa majuto regret) ao masikitiko na imani na kutubu ma zambi yetu, juu ya ile tunasikia pastori, kama vile wakili (Représentant) wa Mungu, anatueleza juu ya mshamasha wa kupitia Bwana wetu na mkombozi Yesu Kristo.

**2. TUNAMPOKEA BWANA WETU**

Kuingia tunaimba zaburi yenye kuchaguliwa tu juu ya kunyanya mioyo ku ibada.

Sifa (Gloria patie ) (P.16) : Tunaomba tena jina la utatu mtakatifu katika Mungu : Mungu Baba, Muumbaji wetu, Mungu Mwana mkombozi wetu, na Mungu Roho

Mtakatifu utakaso wetu, desturi (tradition) lakini sakramenti yenye kuwekwa na Kristo mwenyewe. mwokozi wetu anatuthibitisha kama yeye eko ndani yake.

Kyria (P.17) inakuwa ni msemo yenye kusema kama sisi tuko bure pasipo Mungu na kwa lazima yetu tumu onenyeshe akuje na atujaze na neema yake.

Utukufu ni wa Mungu (Gloria in Exclesis) (P. 17). Tunanyanyuwa sauti zetu kwa Mungu tukimshukuru kwa mtuma mwana wake kuwa mwokozi wetu (hii ni wimbo ulioimbwa na wa malaika wa Bethelemu) Tangu usiku wa kuzaliwa kwake Yesu.

**Salamu (La salutation)** P. 19

Pastori anaomba Roho mtakatifu abariki kanisa (Kusanyiko), kama vile wanatoa sadaka zao na wanatoa akili yao kwa neno lake : “Bwana awe

nanyi". Wote wanajibu wakiomba Roho mtakatifu mwenyewe awe pia kwa Pastori, "nawe pia", ao tena "nawe pia pastori".

**<u>SALA YA SIKU</u> (Collecte de la journée)**

Ni sala mfupi inayoombwa ao kukusanya ( reunir le priere de la journee) mawazo na ma sala ya kanisa mzima kama vile inapatana na somo la siku.

**3. <u>Mungu anatueleza</u>**

Sasa, tunafika pa nafasi ya juu katika kazi yetu. Mbali kama vile tulifunuwa midomo yetu katika sala na kumshukuru Mungu wetu na Bwana. Sasa tunalinda ukimya kwa sababu Bwana wetu mwenyewe atatueleza : atajionyesha yeye mwenyewe na mapenzi yake katika njia moja hasa, tukisoma na tukihubiri neno lake. Mungu anajionyesha yeye mwenyewe

kwetu ndani ya Biblia hii namna moja kupitia ile anatueleza. Hii ni chem – chem ya yote ile tunafundisha na kutumainia. Pasipo neno la Mungu, ibada yetu kama kisima cha imani yetu itapunguka ao kufa.

**Barua (L'Episte)**

Hapa tunasoma mikanda ao barua (epitre) kutoka agano la kale ao agano jipya tunasikia mafundisho ya manabui ; ya yesu kristu na mitume tukiishi maisha ya kikristu.

**Wimbo wa siku (Graduel)**

Inasaidia kipindi cha mpito (transition) kutoka wazo la injili, kama mukiingia unatoka mu zaburi.

**Alleluya** (P. 20)

Maana yake : « Sifa kwa Bwana » ni kipindi kwa mpito ya wazo ya injili. Ni sauti ya furaha ile tuna ruhusiwa nayo kuwa karibu na Bwana wetu.

**Injili**

Injili inasoma katikati ya maisha yetu na maneno ya Bwana wetu Yesu Kristo inakuwa saa yote fungulo ya Neno la siku, ni jambo la lazima ya ukumbusho, ao mafundisho ile tunakumbuka. Kila siku.

**Imani ya Nikea (Credos de Nicée)**

Tulisikia maneno ya Mungu, sasa tuna tangaza ile tunaamini ao kusadiki. Kwa hii tunaonyesha kama dunia, inajaribiwa juu ya

udongo mzuri na kama tulisikia ndani ya somo ya leo kiisha tunaonyesha kazi na matendo na kukatala mafundisho yote mbaya ndani ya imani yetu..

**Wimbo (l'hymne)**

Tunaimbia wimbo ingine juu yakutayarisha mioyo yetu juu ya mwisho wa dunia itakuwa karibu ndani ya mafundisho.

**Mahubiri (Mafundisho) (Le serment)**

Mungu anatueleza kupitia mtumishi wake. Mafundisho ya Pastori aiko wingi wa angalisho, lakini ni mahubiri yenye kutayarishiwa, yenye kujaa na sala na ujumbe (message) wa toba, wokovu wa Mungu na kukomea katika imani.

Wakati ile anapanda kwa mimbari (chaire), Pastori anatulasimu ao (kutulamukia) na salamu ile mtume Paulo alianza kufanya saa yote ndani ya mabarua zake. Ku mwisho wa mafundisho, Pastori anasema : Salamu ya Mungu inayopita akili zote, italinda mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu (Wafilipi 4 : 7). Pastori anawatakia baraka na amani ya Mungu wote walipokea Neno la Mungu.

## 4. TUNAJITOWA KWA BWANA

Tulisikia Neno la Mungu ilisomwa na kufundishiwa. Tulieleza katika rehema yake na baraka yake. Sasa, tunamutolea mioyo zetu na maisha ile anapashwa kubeba na nguvu juu ya kutimiza mapenzi mu mawazo, mu neno na mu matendo.

**Kipindi cha sala (Mkate na Divai (Offertorie)** (P. 22)

Tukitumia maneno ya Daudi ya Toba ya Zaburi ya 51, tunatangaza unyenyekevu wetu katika ungamo la neno na tunajitowa kwa Bwana.

**Sadaka (Zawadi) Offrande**

Tunaleta sadaka yetu ku altare mazawadi hii inaweza kuwa na maana kama tunaitambua katika alama yetu wenyewe kutolewa katika ibada na kazi kwa Bwana.

**Sala (Les prières)**

Tunamuomba Mungu ajaze lazima yetu lazima ya kanisa, na mataifa yote. Katika sala hii tunatowa kutumaini yetu kwa ukohani wa

waamini wote, kwa maana hapa, Pastori asiombe mu jina letu wakati ule tunasikia, lakini masemo yake ni sala il kila mtu kati yetu ndani ya moyo wake anapelekwa kwa upekee kwa Mungu katika jina la Yesu.

**5. BWANA WETU ANAJITOWA YEYE MWENYEWE KWETU SISI**

Sasa, tunakaribia kukipindi cha pili ya ibada yetu, sakramenti ndani ya ile Bwana anakuja kutubariki na mwili na damu. Tunaondoka katika sakramenti na sala ya shukrani na wimbo wa kuabudu.

**Utangulizi (Préface)** P. 24

Mara ingine tena, Pastori na kikundi wanaomba na wanakuwa na akika ya Bwana

Kwa hivi mwaliko (wakunyanywa) mioyo Mungu wetu unakuwa. Hii inatukumbusha uika wetu wote kama vile ibada ya kumushukuru.

**Mtakatifu (Sanctus)** P. 26

Katika wimbo huu tunatukuza na kujiunga pamoja na malaika juu ya kiimbo; mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ku pembeni ya kiti cha enzi cha Bwana na tuna mupokea pamoja na wingi wa watu wa siku ya jumaa ya matawi waliimba mbarikiwa anaye kuja kwa jina la Bwana hosanna kwake juu mbinguni.

**Sala ya Bwana** (P. 27)

Sasa unaomba sala ile Mungu aliotufundisha, sala ya Bwana ni mamlaka ao

mali tafauti ya mkristo. Hapa banatukumbusha kama tuko jamaa ya Mungu, kama ku meza ya Bwana atuna watu wengi, lakini tu mwili moja, ndugu na dada katika imani, ile ya kiroho inajiunga pamoja.

**Maneno ya kuweka** (P. 27)

Hii ni maneno ile Bwana aliyo sema usiku ule alitolewa. Yanafanya ibada ya chakula cha Bwana ya juoni hapana tu kama vile mwili tu ya kutuletea msamaha. Na maneno hii pastori anabariki mkate na divai anaiweka kando kwa matumivu (usage) matakatifu.

**Amani (La paix domini)** P. 27

Pastori anaomba juu Bwana aweze kubariki kanisa na amani yake.

**Mwandoo wa Mungu** **(L'Agnus Dei)** (P. 28)

Tunamuomba Kristo juu atuonyeshe rehema yake.

## 6. TUNAPOKEA CHAKULA CHA BWANA KUGAWANYA

Tunatoka kila upande ndani ya kanisa natuna jipanga kwa musululu na tunaenda ku Altare tunafika na kupiga magoti, juu ya kumpokea Kristo kwa unyenyekevu ndani ya maisha yetu. Kama vile alivyojitowa kwa mara ya kwanza kwetu sisi juu altare ya msalaba (msamaha, maisha, na wokovu) kwa haki yangu.

Wimbo ya Meza ya Bwana

## 7. TUMSHUKURU BWANA WETU

Hi ilikuwa wimbo wa Simeoni ya furaha ndani ya Hekalu wakati alimpokea mototo Yesu kati ya mikono yake, macho yetu iliona vile vile wokovu wa Mungu, kwa sababu tulimpokea Kristo kupitia neno lake na sakramenti. Kama vile Simeoni tunakuwa leo tayari "ya kwenda katika amani".

SHUKRANI P. 30. Tunatowa shukrani yetu ya furaha na sala kwa Mungu.

**Salamu ya baraka** P. 31

Tunajiunga na kanisa la tangu Musa, pastori anafunga ibada. Sauti ya mwisho ile tunasikia kwa midomo yake ni « amani », na alama ya msalaba inatukumbusha hivi wote

weko kwenye msalaba na ustahili wa Kristo Yesu, Bwana wetu, ndani yake tunatumainia na juu yake tunaisha.

**Wimbo wa kufunga (Clôture)**

Sala katika ukimya

Pamoja na akikisho ya baraka ya Bwana juu yetu sisi, na kuwepo kwa nguvu yake inatushindikiza, tunakuwa tayari ya kwenda katika amani ibada yetu kwa Bwana aishe kweli. Tunatoka kanisani katika ibada ya maisha yetu ya kila siku tayari kwa kufanya mapenzi yake. Kwa hiyo jina lake litukuzwe na ufalme wake uje tena kupitia sisi juu ya mapendo ya Yesu.